MKATABA WA AJIRA KWA MADEREVA

Picha ya Mwajiriwa

Makubaliano haya yanafanywa

BAINA YA

……..……...

(ambaye anatambuliwa katika Mkataba huu kuwa ndiye “Mwajiri”)

Anwani ya Mahali alipo, Sanduku la Posta, Simu na Baruapepe ya Mwajiri

…….

……..……...

NA

…….

(ambaye anatambuliwa katika Mkataba huu kuwa ndiye “Mwajiriwa”)

Umri: …… Jinsi: ……...

Anwani ya Mahali alipo, Sanduku la Posta, Simu na Baruapepe ya Mwajiriwa

…….

……..……...

1. KUANZA KUTUMIKA KWA MKATABA

1.1 Mkataba huu Unaanza kutumika tarehe …….. na kuendelea hadi utakapo koma kwa mujibu wa Sheria.

1.2 Ajira hii itakuwa ya masharti ya ……. (***Tafadhali weka alama √ katika kiboksi kimoja kinachohusika***)

- Mkataba usioelezwa muda wa ukomo ☐
- Mkataba ulioelezwa muda wa ukomo (**Kwa wataalam na walio katika kada ya uongozi**) ☐
- Mkataba kwa ajili ya kufanya kazi maalum ☐

2. MAHALI ALIPOAJIRIWA

……..

3. MAHALI PA KAZI

……..

4. MAELEZO KUHUSU KAZI

4.1 Cheo: ……

4.2 Majukumu:……

…….....

5. MATAZAMIO

Mkataba huu utahusisha kipindi cha matazamio cha wiki/miezi …….. kuanzia tarehe ya kuanza kazi. Madhumuni ya kipindi hiki cha matazamio ni kutathmini kama Mwajiriwa ana uwezo

au anafaa kwa kazi hiyo. Pale ambapo Mkataba huu utasitishwa katika mwezi wa kwanza wa ajira, taarifa ya siku saba (7) kwa maandishi itatolewa kwa upande husika.

6. MSHAHARA

6.1 Mshahara wa kuanzia utakuwa shilingi …….. kwa siku/wiki/mwezi (***Kata isiyohusika***).

6.2 Mwajiriwa atakuwa na haki ya posho/malipo yafuatayo kwa fedha taslimu/bonasi/au yasiyo ya fedha;

6.2.1 …… ……

6.2.2 ……..

6.2.3 ……..

……

6.3 Mapato ya ujira wa jumla wa Mwajiriwa yatakuwa ……..…… kwa siku/wiki/mwezi.

6.4 Kipindi cha malipo ya mshahara kitakuwa ni kila wiki/mwezi na mshahara utalipwa kila siku ya …… kama ilivyokubaliwa baina ya Mwajiri na Mwajiriwa.

6.5 Makato katika Mshahara:

6.5.1 Mwajiriwa atakatwa kwa mujibu wa Sheria malipo yafuatayo;

……

……

……

6.5.2 Mwajiriwa amekubali makato yafuatayo;

……

……

7. SAA ZA KAZI

7.1 Muda wa kawaida wa kufanya kazi utakuwa siyo zaidi ya saa **TISA** kwa siku na jumla ya saa **AROBAINI NA TANO** kwa wiki.

7.2 Mwajiriwa atafanya kazi kila siku ya kazi kuanzia saa…….hadi …….; isipokuwa siku ya ……, ambapo atafanyakazi kuanzia saa ….. hadi saa……

7.3 Wiki ya kawaida ya kazi itakuwa siyo zaidi ya siku **SITA.**

7.4 Mwajiriwa atafanyakazi kuanzia siku ya …… na kuishia …… kila wiki; au kwa kadri itakavyokubaliwa baina ya Mwajiri na Mwajiriwa kulingana na mazingira ya kazi.

7.5 Kazi ya saa za ziada (overtime), inaweza kufanywa itakapokubaliwa na Mwajiri na Mwajiriwa.

7.6 Mwajiriwa atalipwa saa za ziada kwa siku za kawaida kwa kiwango kisichopungua mshahara wake kwa saa, ukizidishwa mara moja na nusu, na kuzidishwa kwa jumla ya idadi ya saa za ziada alizofanya kazi.

8. KUFANYA KAZI KATIKA SIKU ZA MAPUMZIKO

Pale ambapo Mwajiriwa atafanya kazi katika siku za mapumziko ya wiki, atalipwa kiwango kisichopungua mara mbili ya mshahara wake kwa saa, ukizidishwa kwa jumla ya idadi ya saa alizofanya kazi.

9. SIKU ZA SIKUKUU

9.1 Mwajiriwa atastahili malipo ya mshahara kama kawaida kwa kila siku ya sikukuu bila kujali kuwa hakufanya kazi.

9.2 Kazi itakayohitajika kufanywa siku ya sikukuu ni lazima iwe kwa makubaliano baina ya Mwajiri na Mwajiriwa.

9.3 Pale ambapo Mwajiriwa atafanya kazi katika siku za sikukuu, atalipwa kiwango kisichopungua mara mbili ya mshahara wake kwa saa, ukizidishwa kwa jumla ya idadi ya saa alizofanya kazi siku hiyo.

10. LIKIZO YA MWAKA

10.1 Mwajiriwa atastahili kupewa likizo yenye malipo ya siku zisizopungua 28 katika kila mzunguko wa likizo ya mwaka. Siku hizi zitajumuisha siku zozote za sikukuu zinazoangukia katika kipindi hicho. “Mzunguko wa likizo ya mwaka”, una maana ya kipindi cha miezi 12 mfululizo tangu Mwajiriwa kuanza ajira yake au tangu kumalizika kwa “mzunguko wa likizo ya mwaka” uliopita.

10.2 Likizo ya Mwajiriwa itachukuliwa kuanzia …… hadi ……. au wakati mwingine kwa kuamuliwa na Mwajiri baada ya kushauriana na Mwajiriwa.

10.3 Idadi ya siku za likizo inaweza kupunguzwa kwa idadi ya siku za likizo ya dharura zilizotolewa kwa maombi ya Mwajiriwa.

10.4 Malipo ya likizo yatatolewa mapema kabla ya kuanza likizo.

10.5 Mwajiri hataamuru au kuruhusu Mwajiriwa kumfanyia kazi wakati wowote wa likizo.

11. LIKIZO YA UGONJWA

11.1 Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 32 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Mwajiriwa atastahili likizo ya ugonjwa yenye malipo, kwa jumla ya siku 126 katika kila mzunguko wa likizo ya ugonjwa, iwapo kama atakuwa na uthibitisho wa vyeti vya daktari kwa kila tukio la kuumwa, wakati atakapohitaji kuchukua likizo ya ugonjwa. Malipo ya mshahara wakati wa likizo ya ugonjwa hayatahitajika kutolewa na Mwajiri iwapo Mwajiriwa anayo stahili nyingine ya likizo ya ugonjwa yenye malipo chini ya Sheria nyingine yoyote, Mfuko au Makubaliano ya Pamoja.

11.2 Malipo ya likizo ya ugonjwa yatakokotolewa kama ifuatavyo:-

(a) Siku 63 za kwanza zitalipwa mshahara kamili,
(b) Siku 63 za pili zitalipwa nusu ya mshahara

11.3 Kwa madhumuni ya likizo ya ugonjwa, “mzunguko wa likizo” ni kipindi cha miezi 36 tangu siku ya Mwajiriwa alipoanza ajira au tangu kuisha kwa mzunguko wa miezi 36 likizo ya mwisho ya ugonjwa.

11.4 Mwajiriwa atamjulisha Mwajiri mapema iwezekanavyo iwapo itatokea kushindwa kufika kazini kutokana na kuugua.

12. LIKIZO YA UZAZI NA ULEZI

Mwajiriwa atakuwa na haki ya likizo ya uzazi (mama) au ulezi (baba) kama inavyoelekezwa na Sheria za Kazi.

13. UKOMO WA AJIRA

13.1 Mkataba huu unaweza kusitishwa kwa upande wowote katika Mkataba huu kuupatia upande mwingine taarifa ya wiki/miezi……..

13.2 Taarifa itatolewa kwa maandishi kwa muda usiopungua kipindi kilichotajwa hapo juu, ikieleza sababu za kusitisha ajira na tarehe ambayo taarifa hiyo imetolewa.

13.3 Wakati wa kusitisha Mkataba, Mwajiri atampatia Mwajiriwa hati inayoelezea utumishi wake (Certificate of Service) kama ilivyoandaliwa katika Sheria/Kanuni.

14. MALIPO YA KIINUA MGONGO

14.1 Pale ambapo Mwajiri atasitisha ajira ya Mwajiriwa; na kwamba Mwajiriwa amemtumikia Mwajiri kwa kipindi kisichopungua miezi 12 mfululizo; Mwajiriwa atastahili malipo ya kiinua mgongo yasiyopungua mshahara wa siku saba kwa kila mwaka aliokamilisha akimtumikia mfululizo Mwajiri, ikizidishwa kwa miaka isiyozidi kumi.

14.2 Mwajiriwa hatastahili malipo ya kiinua mgongo iwapo kuachishwa kwake kazi kulitokana na sababu za;-

14.2.1 Mwenendo wake mbaya, au

14.2.2 Kukosa kwake uwezo, au kutolandana na kazi husika au kutokana na mahitaji ya kiuendeshaji na kama pia Mwajiriwa amekataa kazi au ajira mbadala bila sababu za msingi.

15. MASHARTI MENGINE YA AJIRA AU MAFAO

15.1 Tarehe ya kuajiriwa ni ……..

15.2 Mwajiriwa ataandikishwa uanachama na michango husika kuwasilishwa kwa mujibu wa Sheria katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii aliouchagua, ambao ni……..

15.3 Iwapo Mwajiriwa atasafiri kikazi nje ya kituo chake cha kazi, ndani ya nchi, atastahili kulipwa posho ya kujikimu ya kiasi cha shilingi…… kwa siku.

15.4 Iwapo Mwajiriwa atasafiri kikazi nje ya kituo chake cha kazi, nje ya nchi, atastahili kulipwa posho ya kujikimu ya kiasi cha dola za kimarekani (US Dollars)…..……..… kwa siku.

15.5 Mwajiriwa atalipwa fidia ya madhara (ulemavu na maradhi) yatokanayo na kazi, kama inavyoelekezwa na Sheria.

15.6 Mwajiriwa atastahili huduma ya matibabu ……..

15.7 Mwajiriwa atastahili kukatiwa Bima ya Ajali kwa Dereva na malipo yatatolewa kwake au warithi wake, kwa kuzingatia makubaliano na Mwajiri, iwapo……..

15.8 Mwajiriwa atastahili huduma za mazishi ya staha……..……..

15.9 ……..

15.10 ……..

16. MATUMIZI YA SHERIA

16.1 Mkataba huu utatafsiriwa na kutumiwa kulingana na matakwa ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

16.2 Pale ambapo utatokea mgongano wowote baina ya Mkataba huu na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Matakwa ya Sheria yatatumika kama sehemu ya masharti ya Mkataba huu.

16.3 Mwajiriwa atastahili mafao mengine yoyote yaliyoelezwa na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, hata kama hayakuelezwa katika vipengele vya Masharti ya Mkataba huu au kama ilivyokubaliwa na pande mbili.

IMEWEKWA SAINI:

_____ _____

MWAJIRIWA **TAREHE**

_____ _____

MWAJIRI **TAREHE**

ZINGATIA:

Mkataba huu ni lazima utolewe nakala halisi Tatu zitakazowekwa saini na pande zote mbili; nakala moja anabaki nayo Mwajiri, ya pili anapewa Mwajiriwa na nyingine iwasilishwe SUMATRA.